

Jarida la _____ Toleo Na. 5
SAMIA TENA
04/09/2025 2025-2030



KISHINDO CHA SAMIA MBEYA





RAIS SAMIA: NI MARUFUKU KUZUIA MIILI YA WALIOTANGULIA MBELE YA HAKI KISA HAWAJALIPA

Mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amesema akipata ridhaa ya kuongoza kipindi kingine utakuwa ndo mwisho wa kuzuia miili ya marehemu ambayo ndugu zao wamekosa hela za kulipia matibabu yao.

Dkt. Samia ameyasema leo wakati akihutubia umati mkubwa jijini Mbeya.

Amesema ili kufanikisha hilo serikali itaanzisha mfumo maalumu utakaowezesha wagonjwa au marehemu kulipa kabla na baada ya kupona au kufariki.

Katika hatua nyingine, Rais Samia amesema afya ya uzazi itajumuishwa katika kitita cha Bima ya Afya ili kusaidia wataanzania wote wasio na uwezo kupata huduma bora za uzazi nchini.



DKT. SAMIA KUWEKA TAA ZA BARABARANI KATIKA JIFI LOTE LA MBEYA

Mgombea urais kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameahidi kuweka taa za barabarani katika jiji lote la Mbeya ili kuwezesha vijana kufanya kazi kwa masaa 24.

Akihutubia umati mkubwa jijini humo leo, Rais Samia amesema taa hizo zitawekwa maeneo ya Isae, Meta, njia panda ya Chunya, Uyole na Mbeya mjiini.

Rais Samia amesema taa hizi zitasaidia vijana kujiajiri na kujiongezea kipato iwapo watafanya kazi kwa muda wa masaa 24.





RAIS SAMIA KUKAMILISHA MACHINJIO YA KISASA YA UTENGULE WILAYANI MBALIZI

Mgombea urais kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt Samia Suluhu Hassan ameahidi kukamilisha ujenzi wa machinjio ya kisasa ya Utengule yaliyoko wilaya ya Mbalizi.

Akihutubia maelfu ya wakazi wa Mbalizi leo wakati wa kuomba wananchi ridhaa ya kuongoza kwa kipindi kingine cha miaka mitano, Rais Samia amesema atahakikisha anamaliza kujenga machinjio hiyo ya kisasa ili kuongeza thamani ya nyama ndani na nje ya nchi.

Sambamba na hilo, Rais Samia amesema serikali imeanza zoezi la kutoa chanjo na utambuzi wa wanyama kwa ajili ya kuongezea thamani kuweza kuuzwa nje ya nchi na kuwezesha wafugaji kupata fedha za kigeni na nchi kufaidika kwa ufugaji huo.





RAIS SAMIA: WAKULIMA MSIUZE MBOLEA ZA RUZUKU

Mgombea Urais kupitia Chama cha Mapinduzi(CCM) Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amewaasa watanzania kutouza mbolea za ruzuku wanazopewa bali wazitumie kuzalisha mazao ya kilimo.

Akiongea wilayani Mbalizi wakati akiomba kura, Rais Samia amesema lengo la Kugawa mbolea ya ruzuku ni kuwafanya wakulima kuzalisha kwa wingi na kuuza nje ya nchi.

Sambamba na hilo Rais Samia amewaomba wakulima kuendelea kujisajili na kutunza namba zao za siri. Amesema serikali ina mbolea ya ruzuku ya kutosha ya kupanda na kukuzia na kwa kila zao.

Karibia asilimia 85 ya wakazi wa Mbalizi ni wakulima wa Mahindi, Pareto, Viazi na mazao mengine ambayo kwa kiwango kikubwa yanategemea mbolea ya ruzuku kusitawi.



MGOMBEA SAMIA AAHIDI KUANZISHA VITUO VYA KUNUNUA MAHINDI MWEZI SEPTEMBER SONGWE

Mgombea urais kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan ameahidi kuanzisha vituo vya kununua mahindi Songwe mwezi huu wa Septemba.

Dkt. Samia ameyasema hayo leo Septemba 4, 2025 katika eneo la Mlo, Songwe wakati akihutubia maelfu ya wananchi.

Amesema anajua kuwa kuwa mkoa wa Songwe umezalisha mahindi mengi na hawajaanza kuuza na kuahidi kuanzisha vituo vya kuuza mahindi mwezi huu.





DKT. SAMIA KUANZISHA KONGANI ZA VIWANDA MBEYA

Mgombea urais kupitia Chama cha Mapinduzi(CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan amesema akipata ridhaa ya kuongoza tena kipindi kijacho ataanzisha kongani za viwanda ili kusafirisha mazao ya kilimo yakiwa yameongezwa thamani.

Amesema mazao yatayoongezwa thamani ni yale yanahusu kilimo, mifugo na uvuvi.

Akihutubia umati mkubwa wa watu jijini Mbeya Rais Samia amesema hilo litafanikiwa baada ya kuwa na umeme wa uhakika jijini humu.

Kwa kuanzia Rais amesema serikali itaanza kuwekeza katika kiwanda cha Kokoa ili kukiimarisha.



KINGWENDU NA JB WANASEMA OKTOBA TUNATIKI KINAMNA HII!



SAMIA NI WETU SOTE TUNATAMBA NAYE





DKT. NCHIMBI AINADI ILANI YA CCM 2025 -30 KAHAMA

Mgombea Mwenza wa kiti cha Urais kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM) , Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi, amesema katika miaka mitano ijayo iwapo watanzania watamchagua Mhe. Samia Suluhu Hassan, kama Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali yake itajenga vituo vinne vya afya Kagongwa , Kahama.

Akiongea katika mkutano wa kuomba kura za Urais, wabunge na madiwani kwa ajili ya CCM kwa wakazi wa mji mdogo wa Isaka wilaya ya Kahama Dkt. Nchimbi, amesema kuwa CCM imejipanga kujenga shule za msingi sita na shule za sekondari mbili.

“Kupitia ilani ya CCM 2025 – 2030, iwapo mtatuchagua tuna Kwenda kutekeleza mambo kadhaa hapa Kahama ambapo tutaleta huduma ya maji kutoka ziwa Victoria mpaka hapa Kahama,” Dkt. Nchimbi amesema.

Pia, Dkt. Nchimbi, amesema Serikali ya CCM itajenga visima viwili virefu vitakavyowezesha kuondoa tatizo la upatikanaji wa maji safi na salama.

Aidha, Mgombea Mwenza huyo Dkt. Nchimbi, amesema kuwa mpaka kufikia mwakani Serikali ya CCM itajenga scheme za umwagiliaji maji nne huku wakiendelea kuboresha barabara.



TATIZO LA MAJI KISHAPU KUPATA UFUMBUZI

Mgombea Mwenza wa Urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balizi Emmanuel Nchimbi, ameahidi kuwa endapo chama hicho kitachaguliwa tena kuiongoza nchi, kitajitahidi kuondoa changamoto ya upatikanaji wa maji katika Wilaya ya Kishapu, mkoani Shinyanga.

Ameeleza kuwa Serikali itakayoundwa na CCM itajenga mradi mkubwa wa maji kutoka Ziwa Victoria, ambao utahudumia vijiji 23 vya wilaya hiyo.

Kwa upande wake, mgombea ubunge wa Jimbo la Kishapu kupitia CCM, Lucy Mahyenga, ameomba chama hicho kuwawezesha wadau wa maendeleo kujenga kiwanda kikubwa cha kuchambua pamba na pia kukamilisha baadhi ya miradi ya barabara ambayo ni muhimu katika usafirishaji wa mazao mbalimbali ya chakula na biashara, ikiwemo pamba.



MGOMBEA WETU RAIS DKT. SAMIA AKICHEZA MZIKI KWA FURAHA

Huwezi kuwa na furaha kama mambo yako hayakuendei safi, kama yanaenda fyongo basi huwezi kabisa kuwa na furaha hata ukisema uigize itakushinda tuu, Sasa furaha hupatikana na namna ambavyo wewe mwenyewe utaamua kuishi vizuri ama vibaya na wenzako.

Rais Dkt. Samia amekuwa mwenye kuishi vema na wananchi anaowaongoza kwa maana ya kutekeleza mahitaji yao, kuchapa kazi zenye kuleta tija katika maisha yao na Taifa kwa ujumla.

Hali hiyo imepelekea kupendwa na watanzania wengi na ndio maana hapa Mbeya mjini leo tarehe 4 Septemba 2025, wananchi wakamwambia Mama simama tucheze, wewe ndio jembe letu naye bila kusita kwa furaha aliyonalo akasimama na kucheza mziki pamoja nao.



PROF. KABUDI: JITIHAHA ZA RAIS SAMIA ZAPAISHA ZAO LA PARETO DUNIANI

Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Prof. Palamagamba Kabudi, amesema kuwa jitihada za Rais Samia na mgombea wa nafasi ya Urais kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM), katika kilimo nchini, zimepelekea Tanzania kuwa nchi ya pili katika uzalishaji wa zao la pareto duniani.

Prof. Kabudi ambaye pia ni mbunge wa Kilosa, amesema hayo wilayani Mbalizi, wakati akimuomba kura Rais Samia, wabunge na madiwani kupitia CCM.

“Katika kilimo umefanya mambo makubwa sana hasa kwenye zao la pareto kwani jitihada ulizozifanya kwa kutoa ruzuku na pembejeo zimewezesha Tanzania kuwa nchi ya pili kwa uzalishaji wa zao hilo duniani baada ya Australia. Haya yote yamepatikana ndani ya kipindi cha uongozi wako ambapo naamini kabisa ndani ya miaka mitano ijayo Australia ijiandae kwa kuwa Tanzania inaenda kuwa namba moja kwa uzalishaji wa zao hilo la pareto,” amesema.

Katika upande wa elimu, Prof. Kabudi, amesema Mhe. Samia, amefanya mengi ambapo kwenye shule ya Isalala iliyopo katika kata ya Isalala aliweka jiwe la msingi kwa wanafunzi wenye uhitaji maalumu na kuwagusa walengwa ambao waliimba nyimbo za shukrani kwake kwa mambo aliyoyafanya.

Kutoka hapokwa niaba ya Mhe. Rais, Prof. Kabudi alizindua mradi wa maji Ilula uliogharimu kiasi cha Shilingi bilioni 4.8 ambapo umepunguza adha za upatikanaji wa maji katika eneo hili.





KONA YA ILANI

Kuongeza fursa za ajira kwa vijana, kuongeza kipato kwa wananchi na kupunguza umaskini.



SPIKA TULIA ATAJA SABABU ZA MBEYA KUMCHAGUA RAIS SAMIA

Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Tulia Ackson, ambaye pia ni Mgombea Ubunge Jimbo la Uyole, ameeleza sababu kwa nini wananchi wa Mbeya wamchague Mhe. Samia Suluhu Hassan kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Akieleza juu ya sababu hizo katika mkutano wa kampeni za mgombea Urais kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM) kwenye jimbo la Mbeya Mjini, ametaja kuwa kwenye eneo la afya Mbeya mjini imepata kiasi cha shilingi bilioni 20 ambapo kati ya hizo shilingi bilioni 11 zilienda kwenye hospitali ya Meta huku kiasi cha shilingi milioni 500 zikiwa zimejenga kituo cha afya, shilingi milioni 500 kata ya Itagano zimejenga kituo cha afya, shilingi milioni 500 zimejenga kituo cha afya kata ya Isyesye, na shilingi milioni 500 zimejenga kituo cha afya kata ya Mwakibete.

“Tunazo mashine za kisasa za hospitali ambapo zamani wananchi wetu walikuwa wakifuata huduma hiyo Dar es Salaam sasa hivi huduma hizi za vifaa tiba (MRI) zinapatikana hapa, tuko vizuri na tutaendelea kukuheshimisha,” Dkt. Tulia amesema.

Kwa upande wa elimu, Mhe. Tulia amesema kuwa Serikali imetoa kiasi cha shilingi bilioni 31.1 ambazo zimetuwezesha kupata shule ya msingi na sekondari, nakuongeza kuwa Mbeya ni moja ya sehemu ya nchi ambayo ina vyuo vingi ambapo vijana wengi wanapata mikopo.

“Ndugu zangu wanambeya nayasema haya kama sehemu ya utekelezaji wa ilani ya CCM 2020 – 2025 natengeneza njia ya hesabu ya kwa nini tumpe kura za ushindi lakini si tu ushindi ila kura za heshima kwa kuwa ametuheshimisha,” Mhe. Dkt. Tulia amesema.

TABASAMU LA MAMA



KUTOBA



KUFAKILI



*Kazi na Utu
Tunasonga Mbele*

ssh_anatekeleza